

# TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA NANSIO (“NANSIO WSSA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-049

Mnamo tarehe 2 Mei 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Nansio (Nansio WSSA) la kutaka kurekebisha bei za huduma za majisafi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Jedwali hapa chini linnaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

**Jedwali: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)**

Kundi la Wateja	Kiwango cha Matumizi (mita za ujazo)	Bei za Sasa	Proposed Tariff					
		2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21	Badiliko	2021/22
Majumbani	0-7	725	141%	1,750	6%	1,850	5%	1,950
	8-14	725	141%	1,750	6%	1,850	5%	1,950
	=>15	725	141%	1,750	6%	1,850	5%	1,950
Taasisi	-	840	114%	1,800	11%	2,000	10%	2,200
Biashara	-	1,180	69%	2,000	10%	2,200	9%	2,400
Viwandani	-	1,415	55%	2,200	9%	2,400	8%	2,600
Magati	-	1,200	17%	1,400	7%	1,500	10%	1,650
Ujenzi	-	1,200	9%	1,305	53%	2,000	25%	2,500

Kwa mujibu wa wasilisho la WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ya kutosha kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo. Aidha, Mamlaka ya maji Nansio imebainisha kuwa mabadiliko ya bei yanayopendekezwa yataiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji zilizoongezeka, kuboresha huduma za maji safi ikiwa ni pamoja na kuongeza mtandao wa majisafi na kufanya uwekezaji wa miundombinu ya maji na hivyo kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Nansio.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 26 Juni 2019, katika Ukumbi wa Halmashauri ya**

**Wilaya Ukerewe** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe **2 Julai 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA Kanda ya Ziwa, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF, MTAA WA KENYATTA, S.L.P 2069 MWANZA** au **Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira NANSIO** zilizopo mjini Nansio.

**Imetolewa na:**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**  
**12 Juni 2019**

